



## MAREJESHO YA MALIPO YA BIMA YA AFYA KWA WAHITIMU WA IFM

CHUO CHA USIMAMIZI WA FEDHA (IFM) KINAWATANGAZIA WANAFUNZI WALIOHITIMU AMBAO HAWAJAOMBA KUREJESHEWA FEDHA WALIZOLIPA KWA AJILI YA KUPATIWA VITAMBULISHO VYA BIMA YA AFYA WAKATI TAYARI WALIKUWA NA KADI HIZO, KUWASILISHA MAOMBI YA KUREJESHEWA FEDHA ZAO. TANGAZO HILI LINAWAHUSU PIA WAHITIMU AMBAO WANASTAHILI KURUDISHIWA FEDHA HIZO KUTOKANA NA SABABU NYINGINEZO.

UNAPOFANYA MAOMBI YA KUREJESHEWA MALIPO HAYO UNATAKIWA KUAMBATANISHA VITU VIFUATAVYO:

1. MAJINA YAKO KAMILI KAMA ULIVYOJISAJILI CHUONI,
2. AKAUNTI NAMBA NA JINA LA BENKI,
3. NAMBA YAKO YA SIMU.

MAREJESHO YATAFANYIKA KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA TOKEA TAREHE YA TANGAZO HILI. BAADA YA MUDA HUO KUPITA HAKUNA ATAKAYEREJESHEWA MALIPO HAYO.

MAJINA YA WANAOSTAHILI KUREJESHEWA YANAPATIKANA KATIKA TOVUTI YA CHUO: <http://www.ifm.ac.tz>

**IMETOLEWA NA;**

**NAIBU MKUU WA CHUO.**

*All correspondence should be addressed to the Rector*

5 Shaaban Robert Street, Post Code: 11101, P. O. Box 3918, Dar es Salaam – Tanzania,  
Tel: +255222112931-4, Fax: +255222112935, Email: [rector@ifm.ac.tz](mailto:rector@ifm.ac.tz), Website: [www.ifm.ac.tz](http://www.ifm.ac.tz)

**JIFUNZE UHUDUMIE**

